# Fedha zinamiminika, maji kiduchu

## Changamoto za upatikanaji wa maji safi nchini Tanzania





## 1. Utangulizi

Upatikanaji wa maji safi na salama ni changamoto kubwa kwa watu wengi nchini Tanzania. Ingawa kimataifa, Malengo ya Maendeleo ya Milenia (MDG) ya usambazaji wa maji yamefikiwa, upatikanaji wa maji safi nchini Tanzania umezorota. Kwa miongo kadhaa nchi imekuwa nyuma zaidi ya nchi nyingine ambazo ziko kwenye ngazi sawa kimaendeleo na kijiografia.

Changamoto ya upatikanaji wa maji safi inaendelea kuwepo pamoja na uwekezaji mkubwa katika miaka ya hivi karibuni. Serikali ya Tanzania hivi karibuni imehusisha jitihada zake za kuboresha upatikanaji wa maji safi na salama kwa wananchi vijijini, jitihada hizo zikiwa ni pamoja na kupitia Mpango wa *Matokeo Makubwa Sasa*[1] . Lengo kuu ni kutoa huduma ya maji kwa zaidi ya watu milioni 15.4 wanaoishi maeneo ya vijijini, hatua ambayo itakuza asilimia ya watu wanaopata maji safi kuwa 75% ifikapo mwaka 2015 . Matokeo ya utafiti katika muhtasari huu, ambayo yanawakilisha takwimu za hivi karibuni za kitaifa za upatikanaji wa maji safi, yanaonesha kuwa jitihada hizo ziko ndani ya wakati, ingawa malengo ni makubwa na yanaweza yasifikiwe kutokana na ukubwa wa changamoto yenyewe.

Matokeo haya yametokana na awamu sita za *Sauti za Wananchi*, utafiti wa kwanza barani Afrika wenye uwakilishi wa kitaifa unaofanyika kwa njia ya simu mkononi. Simu zilipigwa kati ya tarehe 7 na 13 Agosti 2013; na takwimu hizi ni pamoja na majibu kutoka kaya 1,702. Muhtasari huu pia unatoa matokeo kutoka moduli ya maji y a utafiti wa awali wa *Sauti za Wananchi* ambao ulifanyika kati ya mwezi Oktoba 2012 na Januari 2013 na kuzifikia kaya 2,000, Pia Program ya Pamoja ya Ufuatiliaji (JMP) wa Usambazaji wa Maji na Usafi wa Mazingira ya Shirika la Afya Duniani (WHO) na Shirika la kuhudumia watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF), na utafiti wa Afrobarometer wa mwaka 2012.

1 "Matokeo Makubwa Sasa (BRN) ni Mpango unaolenga kutumia mbinu mpya ya kufanya kazi kwa kipindi maalumu kuleta ufanisi wa utoaji huduma kwa hatua za mabadiliko yanayohitajika", ukijikita kwenye maeneo sita ya vipaumbele vya uchumi, maji ni kipaumbele mojawapo (http://www.pmoralg.go.tz/quick-menu/brn/).

2 Kauli ya Mhe. Jumanne Maghembe, Waziri wa Maji, katika makala iliyochapishwa na African Review of Business and Technology, "Tanzania kuzindua miradi ya maji zaidi ya 1,800 ," 25 Aprili 2013. http://www.africanreview.com/manufacturing/water-a-environment/tanzania-to-launch-more-than-1-800-projects-to-battle-water-woes

Muhtasari huu umeandikwa na kuchapishwa na Twaweza, iliyopo Hivos Tanzania. Umetolewa mwezi Aprili 2014

S.L.P 38342, Dar es Salaam, Tanzania.
Simu: +255 22 266 4301 Nukushi: +255 22 266 4308.
uwazi@twaweza.org www.twaweza.org/sauti

Twaweza ni sisi

Matokeo muhimu ni:[3]


- Upatikanaji wa maji safi nchini Tanzania umezorota na kupungua katika miongo miwili iliyopita, kinyume na mwelekeo chanya (kuboreka kwa huduma ya maji) kikanda, licha ya uwekezaji mkubwa kwenye maji kufanyika.
- Karibu theluthi moja ya Watanzania wanasema kuwa changamoto za usambazaji maji ni miongoni mwa matatizo matatu makubwa zaidi yanayoikabili nchi yetu leo.
- Idadi kubwa ya Watanzania (89%) wanapata maji kwa ajili ya mahitaji yao ya kila siku kutoka vyanzo vya maji vya umma. Hii inawachukua saa moja au zaidi - ambayo ni mara mbili ya lengo rasmi la Serikali la kutumia dakika 30.
- Wanawake na wasichana wana jukumu la msingi la kutafuta maji kwa ajili ya mahitaji ya kila siku ya kaya zao.

# 2. Mambo saba kuhusu upatikanaji wa maji safi nchini Tanzania

## Jambo la 1: Tanzania iko nyuma kati ya nchi zingine barani Afrika

Asilimia ya watu wanaotumia maji safi na salama kwa ajili ya kunywa imeongezeka katika nchi nyingi barani Afrika tangu takwimu za ulinganifu zilipoanza kukusanywa - kutoka 49% mwaka 1990 hadi 63% mwaka 2011[4]. Kimsingi hii inaonyesha ongezeko la upatikanaji wa maji kwa wananchi wa vijijini, ambao umepanda kutoka 35% hadi 51%. Hata hivyo, takwimu kuhusu Tanzania zinaeleza hali tofauti. Kwa ujumla, upatikanaji wa maji safi na salama katika miongo miwili iliyopita umepungua kidogo kutoka 55% hadi 53%, na kwa wananchi wa vijijini, imeshuka kutoka 46% hadi 44%. Kama inavyooneshwa katika Kielelezo cha 1, malengo ya Matokeo Makubwa Sasa ya kufikia 75% ifikapo mwaka 2015 itahitaji maboresho makubwa kutokana na mwenendo wa usambazaji maji ulivyo sasa. Tanzania inahitaji kufikia lengo hilo katika kipindi cha miaka miwilimpaka mitatu kitu ambacho nchi za Afrika kwa wastani zimeshindwa kufikia kwa kipindi cha miaka 20 iliyopita.

**Kielelezo cha 1: Asilimia ya watu wanaotumia vyanzo (vilivyoboreshwa) vya maji safi ya kunywa**




**Chanzo cha takwimu:**WHO/UNICEF Mpango wa Pamoja ya Ufuatiliaji wa Usambazi Maji na Usafi wa Mazingira.

---

3 Kwa ajili ya kusomeka mihutasari ya ripoti za Sauti za Wananchi hazijaweka wastani wa uwiano wa takwimu zilizotumika. Hata hivyo, zinapatikana kwa kuombwa na mtumiaji.


4 Asilimia hizi zinaonesha uwiano wa idadi ya watu wanaotumia chanzo 'kilichoboreshwa' cha maji ya kunywa, ambacho kinaweza kuwa kati ya hivi vifuatavyo: maji ya bomba nyumbani, bomba la maji la umma, au bomba la kupampu, kisima duara/kisima kirefu, kisima kilichojengewa, chemchem iliyohifadhiwa, au maji ya mvua.

Takwimu kutoka utafiti wa awali wa *Sauti za Wananchi* zinathibitisha matokeo ya Mpango wa Pamoja ya Ufuatiliaji (JMP)wa Ugavi wa Maji na Usafi wa Mazingira ya WHO/UNICEF. Kwa mujibu wa utafiti huu wa hivi karibuni , asilimia 54 ya Watanzania wote hupata maji ya kunywa kutoka katika chanzo 'kilichoboreshwa'; hata hivyo takwimu kwa wakazi wa vijijini bado ziko chini kwa kiwango cha 42%.[5]

## Jambo la 2: Ongezeko la bajeti na misaada halionekani

Upatikanaji wa maji safi na salama kunastusha ikilinganishwa na ongezeko la matumizi ya bajeti katika sekta ya maji. Kielelezo cha 2 kinapingana na matumizi "halisi" ya kila Mtanzania. Matumizi ya maji yaliyowianishwa na mfumuko wa bei tangu 1999/2000 na asilimia ya watu wanaotumia chanzo safi na salama cha maji ya kunywa. Ongezeko kubwa la bajeti ya maji kwa kila Mtanzania kutoka chini Tsh 1,000 hadi zaidi ya Tsh 3,000 katika miaka kumi iliyopita wakati hakuna maboresho linashangaza.

**Kielelezo cha 2: Matumizi kulinganisha na upatikani wa maji**





**Chanzo cha takwimu:** Mapitio ya Matumizi ya Fedha za Umma (PER) ya Sekta ya Maji, 2009; Tanzania PER 2010; 2013 Overseas Development Institute: Uchambuzi wa haraka wa Sekta ya Maji nchini Tanzania; Hesabu za Taifa za Tanzania Bara 2011; Viashiria vya Maendeleo duniani vya Benki ya Dunia; Takwimu za mabadiliko ya bei za watumiaji za Benki ya Dunia /Shirika la Fedha la Kimataifa

Ni muhimu kufahamu kwamba Tanzania pia inapata misaada mingi na mikubwa kuliko nchi jirani ambayo inatolewa hasa kwa ajili ya usambazaji wa maji kwa kila anayenufaika na usafi wa mazingira, lakini haina mengi ya kuonesha kuthibitisha hilo katika suala la idadi ya watu wanaofikiwa na huduma hizo. Kwa kipindi cha miaka 10 ya tangu 1995 mpaka 2005, Tanzania ilipokea misaada ya sawa na dola za Kimarekani 57 kwa kila anayenufaika ambayo iliyotolewa kwa ajili ya maji lakini upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama ulipungua kwa 1%. Ethiopia, Kenya na Uganda wote walipokea misaada pungufu ya kiasi ilichopokea Tanzania lakini ziliweza kuboresha upatikanaji wa maji sehemu kubwa ya wananchi wao,

5 Takwimu hizi zinahusu msimu wa kiangazi. Zaidi ya nusu ya sampuli (60%) wanatumia chanzo kilekile cha maji msimu wa mvua; kwa wale wanaotumia chanzo tofauti, idadi ya wanaopata maji kutoka chanzo bora kwa ujumla iko juu yapata - 70% na kwa wakazi wa vijijini ni 63%. Kuna uwezekano wa Takwimu hizi za juu kuwa zimetokana na ukweli kwamba maji ya mvua huchukuliwa kama chanzo cha maji 'kilichoboreshwa' kwa mujibu wa JMP.

kama inavyooneshwa katika Kielelezo 2a.

**Kielelezo cha 2a: Misaada kwa ajili ya Maji ikilinganishwa na mabadiliko ya upatikanaji wa maji**





**Chanzo cha takwimu:** *African Ministers' Council on Water* (AMCOW) Ripoti za Nchi kwa Mikoa

## Jambo la 3: Upatikanaji wa maji safi unaonekana kuwa tatizo kubwa

Haishangazi, kutokana na takwimu hizi, karibu theluthi moja (30%) ya Watanzania wanaliweka tatizo la kukosekana kwa maji safi na salama kuwa ni moja ya matatizo matatu makubwa zaidi yanayoikabili nchi leo. Uwiano ni wa juu kidogo kwa wakazi wa vijijini (33%) kuliko wakazi wa mijini (26%). Matatizo mengine makubwa ya utoaji huduma yaliyotajwa na Watanzania wengi ni pamoja na huduma za afya (30%) na elimu (24%).[6]

**Kielelezo cha 3: Ni matatizo gani makubwa zaidi yanayoikabili nchi yetu?**





**Chanzo cha takwimu:** Utafiti wa awali wa *Sauti za Wananchi*, Oktoba-Desemba 2012.

6 Matokeo haya yameoana na yale ya utafiti wa Afrobarometer wa mwaka 2012, ambao ulibaini kuwa 35% ya Watanzania waliripoti kuwa tatizo la maji ni miongoni mwa matatizo matatu makubwa yanayoikabili nchi ambayo Serikali inapaswa kuyashughulikia.

## Jambo la 4: Upatikanaji wa maji safi ni changamoto ya kila siku

Hata wale ambao wanamudu kupata maji ya kunywa kutoka vyanzo safi na salama wanakabiliwa na changamoto ya kupata huduma hiyo kila siku. Zaidi ya Watanzania watatu kati ya wanne (76%) wanakiri kuwepo kwa changamoto za za aina mbalimbali za upatikanaji wa maji. Changamoto kubwa inayotajwa na idadi kubwa ya wakazi mijini na vijijini ni umbali wa kuvifikia vyanzo vya maji. Hata hivyo hili linaonekana kuwa ni tatizo zaidi kwa maeneo ya vijijini. Changamoto kuhusiana na utoaji huduma wa vyanzo vya maji ziko katika maeneo ya mijini na vijijini, kama zilivyo changamoto zinazohusiana na uhaba wa vyanzo vya maji (miundombinu). Gharama ya maji pia imetajwa kuwa changamoto zaidi kwa wakazi wa mijini.

**Kielelezo cha 4: Matatizo yanayohusiana na upatikanaji wa maji safi**





**Chanzo cha takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 6, Agosti 2013.

## Jambo la 5: Watu wengi hupata maji kutoka vyanzo vya umma

Kutoridhika kwa watu kuhusu huduma za maji inaweza kuonyesha changamoto zinazowakabili katika upatikanaji wa maji safi kwa matumizi ya kila siku. Watanzania wengi (89% ya kaya) hupata maji kwa ajili ya mahitaji yao ya kila siku kutoka katika vyanzo vya umma, ikilinganishwa na 7% ambao wana bomba binafsi nyumbani au bomba la maji kuwepo ndani ya maeneo yao na 4% wanatumia maji ya kuletewa[7]. Zaidi ya kaya nne kati ya tano (81%) ambazo wanapata maji kutoka kwenye bomba au kuletewa na watu au magari wanaishi maeneo ya mijini.

[7] Takwimu hizi ni za msimu wa kiangazi; takwimu za msimu wa mvua (masika) zinafanana sana: Wenye mabomba nyumbani ni 6%, wanaopata maji kutoka vyanzo vya umma 91%na wanaoletewa ni 3%.

**Kielelezo cha 5: Namna ya kupata maji**





**Chanzo cha takwimu:** Utafiti wa awali wa *Sauti za Wananchi,* Oktoba-Desemba 2012.

## Jambo la 6: Kuchota maji kunatumia muda mwingi

Watu wanaotafuta na kuchota maji kwa ajili ya mahitaji yao ya kila siku, inawachukua wastani wa saa moja (dakika 57) kupata maji ya kunywa kutoka kilipo chanzo cha maji cha umma mpaka kwenye makazi yao[8] - hii ni mara mbili ya lengo rasmi la muda uliopangwa na Serikali wa dakika 30 kukamilisha uchotaji maji na kuyafikisha nyumbani[9]. Watu kwa kawaida hutumia takribani nusu ya muda huu (dakika 24) kusubiri katika foleni kwenye chanzo cha maji. Muda wa kusubiri unaweza kuwa zaidi ya mara tatu (dakika 79) kipindi cha uhaba wa maji.

**Kielelezo cha 6: Muda unaotumika kuchota maji (dakika)**




**Chanzo cha takwimu:** Utafiti wa awali wa *Sauti za Wananchi,* Oktoba-Desemba 2012.


8 Haya ni makadirio kwa kipindi cha kiangazi; Utafiti wa Awali wa SzW haukuhoji kuhusu kipindi cha masika.

9 Kwa mujibu wa Mkakati wa Kitaifa wa Maendeleo ya Sekta ya maji wa mwaka 2005 (NWSDS): " Mkakati wa viwango vya huduma utakuwa … ili kuhakikisha kuwa chanzo chochote cha maji kinatumiwa na watu si zaidi ya 250 kikiwa umbali usiozaidi mita 400 kutoka kwa watumiaji walio mbali zaidi, na watumiaji wachukue dakika 30 kukamilisha safari moja ya uchotaji maji".

### Jambo la 7: Wanawake na wasichana wana jukumu la msingi la kuchota maji

Wanawake na wasichana wana wajibu mkubwa wa kuchota maji kwa ajili ya familia zao. Hususan, 73% ya kaya zinazochota maji kwa ajili ya mahitaji yao ya kila siku (badala ya maji kutoka kwenye mabomba au kuletwa), mkuu wa kaya mwanamke ndiye mwenye jukumu la kufanya kazi hii.[10]

**Kielezo cha 7: Nani huchota maji?**




**Chanzo cha takwimu:** Utafiti wa awali wa *Sauti za Wananchi,* Oktoba-Desemba 2012.

## 3. Hitimisho

Muhtasari huu unatoa tathmini ya kimahesabu ya upatikanaji wa maji safi nchini Tanzania. Takwimu kutoka utafiti kwa njia ya simu za mkononi wa *Sauti za Wananchi* zinaonyesha kuwa upatikanaji wa maji safi unaonekana kuwa ni moja ya matatizo makubwa zaidi yanayoikabili Tanzania leo. Kaya nyingi huchota maji kutoka chanzo umma, ambapo inachukua wastani wa saa moja kukamilisha safari moja ya uchotaji maji. Pia uchotaji maji karibu siku zote hufanywa na wanawake na wasichana. Kwa sababu maji safi ni hitaji la msingi na linachangia ulindaji afya, hasa kwa watoto wadogo, ni wazi kuwa upatikanaji wa maji ni kipaumbele cha sera Tanzania.

Licha ya kuongezeka mara tatu kwa bajeti ya matumizi ya maji kati ya mwaka 2000 na 2012, upatikanaji wa vyanzo vya maji safi haujaboreka kihalisia, kiwango cha usambazji maji kimepungua kidogo katika kipindi hiki. Ukizingatia ukweli kwamba hakuna uhusiano mzuri kati ya matumizi na utoaji wa huduma katika sekta ya maji nchini Tanzania kunaibua swali kubwa kuhusu maamuzi ya kisera na uwajibikaji. Kiasi kikubwa cha fedha za ziada kilitengwa na kutolewa katika kipindi cha miaka ya hivi karibuni: fedha hii yote ilikwenda wapi na kwa sababu gani upatikanaji wa maji haukuongezeka? Kupanga na kufunga pampu ya kijijii

---

[10] Asilimia hizi zikijumlishwa pamoja zinazidi 100% kwa sababu kaya ziliweza kutoa jibu zaidi ya moja kwenye swali hili.

kunaweza kuchukua hadi mwaka mmoja: hivyo, kwanini ongezeko kubwa la rasilimali, hasa kati ya mwaka 2003 na 2007, halikusababisha uanzishaji wa vyanzo vya maji sehemu kubwa ya nchi?

Katika miaka ya hivi karibuni mipango kadhaa mipya katika sekta ya maji imeanzishwa. Tangu uzinduzi wa Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Maji mwezi Julai 2007, Serikali ya Tanzania na wafadhili wake wametumia zaidi ya dola milioni 900 (karibu shilingi bilioni 1.5) kushughulikia changamoto zinazohusiana na upatikanaji wa maji safi, lakini mafanikio ya kuonesha ni madogo sana[11]. Je, mpango wa Matokeo Makubwa Sasa utawakilisha mabadiliko makubwa? Wakati jitihada mpya na umakini katika sekta ya maji vinakaribishwa, Serikali bado haijatoa mipango yenye maelezo ya kina kwa ajili ya kufanikisha matokeo tarajiwa, hili litaweka ugumu katika kufuatilia hatua za maendeleo. Kwa mfano, ahadi iliyotolewa kama sehemu ya Mpango wa Kimataifa wa Kuendesha shughuli za Serikali kwa Uwazi (OGP)[12] ya kuweka wazi takwimu za maeneo ya vyanzo vya maji kwenye mtandao haijatimizwa kikamilifu. Kwa ujumla, haiko wazi kama mipango mipya imeandaliwa kwa kuzingatia ushahidi, na kama kuna mfumo wa uwazi wa kutosha na uwajibikaji kuhakikisha thamani ya fedha inapatikana.

Matokeo yaliyotolewa hapo juu yanaweka wazi ukubwa wa changamoto ya upatikanaji wa maji safi nchini Tanzania. Yanaonesha haja ya kuweka vipaumbele vya wazi; kutafakari kwanini juhudi za nyuma za kuboresha upatikanaji wa maji zilishindwa kwa kiasi kikubwa; kufikiria upya sera za sasa na utendaji katika sekta kwa kuzingatia ushahidi mathubuti kuhusu masuala ya kiufundi na kiutawala; na kuhakikisha kuna uwazi mkubwa katika ngazi zote. Vinginevyo, changamoto ya upatikanaji wa maji ina uwezekano wa kuendelea kuwepo, huku ikipanua pengo kati ya Tanzania na majirani zake nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, na kushindwa kutimiza matarajio ya mamilioni ya watu na hasa wanawake na watoto nchini kote.

---

11 Awamu ya Kumi ya Mpango wa Usimamizi wa Pamoja, program ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, Mei 20 - 31, 2013, Kitabu cha kumbukumbu.

12 Ahadi 3.4 (i) kwenye Mpango wa Uwazi Serikalini nchini wa 2012-3 http://ow.ly/uYxpK (ilichukuliwa 12 Machi 2014)